FUNZO LA 2

1. Kwa nini nilikuja hapa?
-Kukuambia ujumbe muhimu zaidi ulimwenguni.

2. Ni ujumbe wa nani ulio muhimu zaidi ulimwenguni?
-Ujumbe wa Mungu.

3. Kwa nini ujumbe wa Mungu ndiyo ujumbe muhimu zaidi ulimwenguni?
-Kwa sababu ni Mungu pekee ambaye hajawahi kudanganya.
-Kwa sababu ni Mungu pekee ambaye amekuwa akisema ukweli wakati wote.

4. Ujumbe wa Mungu uko wapi?
-Ujumbe wa Mungu umo katika kitabu cha Mungu.

5. Jina la kitabu cha Mungu ni lipi?
-Jina la kitabu cha Mungu ni Biblia.

6. Ujumbe wa Mungu uliingia aje katika kitabu cha Mungu?
-Hapo zamani, Mungu aliwachagua baadhi ya watu, kisha akatia maneno yake katika mawazo ya hao watu.
-Kisha hao watu wakayaandika maneno ya Mungu ndani ya kitabu cha Mungu.

7. Je, watu hao waliandika maneno yao katika kitabu cha Mungu?
-La.
-Hao watu, ambao Mungu aliwachagua, waliyaandika maneno



ya Mungu hakika kama vile walivyoambiwa na Mungu.

8. Je, watu hao, ambao waliandika maneno ya Mungu, waliishi kwa wakati mmoja?
-La.

9. Je, ilichukuwa muda wa miaka mingapi kuandika maneno yote ya Mungu?
-Miaka 1,600.

10. Je, watu hao ambao Mungu aliwachagua kuyaandika maneno yake walikuwa nani?
-Watu ambao Mungu aliwachagua kuyaandika maneno yake walikuwa Wayahudi na Myunani.

11. Watu hao waliyaandika maneno ya Mungu katika lugha gani?
-Katika lugha za Kiyahudi na Kiyunani.

12. Ni maneno mangapi ya Mungu katika kitabu cha Mungu ambayo ni ya kweli?
-Yote.

13. Kwa nini maneno yote ya Mungu katika kitabu cha Mungu ni ya kweli?
-Kwa sababu kamwe Mungu hadanganyi.
-Kwa sababu Mungu husema ukweli tu.

-Maneno ya kwanza ambaye Mungu aliyaandika katika kitabu chake ni yapi?

-Maneno ya kwanza ambaye Mungu ameyaandika katika kitabu chake ni:

-“Hapo mwanzo.”

-Kwa nini maneno ya Mungu ya kwanza ni, “Hapo mwanzo”?

-Kwa sababu Mungu anataka tujue kuwa kila kitu kina mwanzo.

-Je, kila kitu tunachokiona, kina mwanzo?
-Ndiyo.

-Je, kila kitu tusichokiona kina mwanzo?
-Ndiyo.

-Je, maisha yalikuwaje kabla ya mwanzo?

-Kabla ya mwanzo, kulikuweko mito au ziwa?
-La.
-Kabla ya mwanzo, kulikuweko milima au miti?
-La.

-Kabla ya mwanzo, kulikuweko jua, mwezi au nyota?
-La.
-Kabla ya mwanzo, kulikuweko wanyama au ndege?
-La.

-Kabla ya mwanzo, kulikuweko dunia au anga?
-La.



-Kama hivi vyote havikuwa kabla ya mwanzo, je, unafikiri kuwa watu walikuepo kabla ya mwanzo?
-La.

-Kama ziwa, miti, jua, anga na dunia havikuwepo kabla ya mwanzo, watu wengeweza kuishi?
-La.

-Kabla ya mwanzo, kulikuwepo wazungu au watu weusi?
-La.
-Kabla ya mwanzo, roho zilikuwepo?
-La.

-Kabla ya mwanzo, hakukuwa na chochote.

-Wacha tusome tena maneno ya kwanza ya Mungu katika kitabu chake:
-“Hapo mwanzo, Mungu.”

-Je, maneno ya kwanza ya Mungu yanasema nini?

-Maneno ya kwanza ya Mungu yanasema kwamba, kabla ya mwanzo, kulikuweko na Mungu pekee.

-Ni nani pekee aliyekuwa anaishi kabla ya mwanzo?
-Mungu.

-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo, ni nani aliye mkuu zaidi ya kila kitu?
-Mungu.

-Mungu ni mkuu zaidi ya mito na ziwa.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo.

-Mungu ni mkuu zaidi ya milima na miti.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo.

-Mungu ni mkuu zaidi ya jua, mwezi au nyota.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo.

-Mungu ni mkuu zaidi ya dunia na anga.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo.

-Mungu ni mkuu zaidi ya watu wote ulimwenguni.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo.

-Mungu ni mkuu zaidi ya roho zote ulimwenguni.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo.

-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo, ni nani peke yake anayeweza kutuambia kuhusu mwanzo?

-Mungu.
-Kwa nini watu hawawezi kutuambia kuhusu mwanzo?
-Kwa sababu watu hawakuwa wakati huo.



-Kwa nini roho haziwezi kutuambia kuhusu mwanzo?
-Kwa sababu roho hazikuwepo wakati huo.

-Mungu alianza lini?

-Mungu hana mwanzo.
-Mungu amekuwa hai wakati wote.
-Mungu ni wa milele.

-Kuna watu wanaofikiria kuwa Mungu alizaliwa na mtu.

-Je, kuna aliyemzaa Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

-Kuna wanaofikiria kuwa Mungu alijizaa mwenyewe.

-Je, Mungu alizaa Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

-Kuna wanaofikiria kuwa Mungu alitengenezwa na watu.

-Je, kuna aliyemtengeneza Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

-Kuna wanaofikiria kuwa Mungu alijitengeneza mwenyewe.

-Je, Mungu alitengeneza Mungu?

-La.
-Mungu ni wa milele.

-Je, kulikuwepo wakati ambapo Mungu hakuwepo?
-La.

-Mungu amekuwa hai wakati wote.
-Mungu atakuwa hai wakati wote.

-Mungu amekuwepo wakati wote.
-Hakuna wakati ambapo Mungu hakuwepo.

-Mungu hawezi kufa.
-Mungu hawezi hisi njaa.
-Mungu hawezi hisi kiu.

-Watu wanaitaji maji na chakula ili waishi je, Mungu anaitaji nini ili aishi?
-Mungu haitaji chochote ili aishi.

-Mungu anaishi vipi?
-Kwa nguvu zake mwenyewe.

-Kwa nini Mungu haitaji dunia ili atembee juu yake?
-Kwa sababu Mungu anaishi kwa nguvu zake mwenyewe.

-Kwa nini Mungu haitaji jua ili aone?
-Kwa sababu Mungu anaishi kwa nguvu zake mwenyewe.

-Kwa nini Mungu haitaji chakula ili ale?



-Kwa sababu Mungu anaishi kwa nguvu zake mwenyewe.

-Kwa nini Mungu haitaji maji ya kunywa?
-Kwa sababu Mungu anaishi kwa nguvu zake mwenyewe.

-Je, waweza kuishi bila dunia au jua?
-La, lakini Mungu anaweza.

-Je, waweza kuishi bila chakula au maji?
-La, lakini Mungu anaweza.

-Mungu si kama wanadamu.
-Mungu si kama wanyama.
-Mungu si kama maroho.

-Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo, Mungu haitaji chochote.

-Ni nani aliye mkuu zaidi ya jua, mwezi na nyota?
-Mungu.

-Ni nani aliye mkuu zaidi ya anga na dunia?
-Mungu.

-Ni nani aliye mkuu zaidi ya watu wote na maroho yote?
-Mungu.

-Hakuna kitu chochote kikubwa zaidi ya Mungu.
-Hakuna aliye mkuu zaidi ya Mungu.